JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
BODI YA KAHAWA TANZANIA

*(Imeanzishwa kwa Sheria ya Kahawa Namba 23 ya Mwaka 2001 na Marekebisho ya Sheria za Mazao Na. 20 ya mwaka 2009)*

# TAARIFA KWA UMMA

## KUH: TANGAZO LA MAOMBI YA KUOMBA UWEZESHAJI WA MASHINE ZA KUCHAKATA KAHAWA (PULPING MACHINES)

**1.0. UTANGULIZI**

Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) inapenda kuzijulisha AMCOS zinazolima kahawa kuwa imefungua dirisha la kupokea maombi ya uwezeshaji wa mashine za kuchakata kahawa (Pulping Machines). Lengo la mpango huu ni kuimarisha shughuli za uchakataji wa kahawa ili kuongeza ubora wa kahawa inayozalishwa nchini na hivyo kuongeza mapato ya wazalishaji wa kahawa.

**2.0 UTARATIBU WA UOMBAJI WA MASHINE ZA KUCHAKATA KAHAWA (PULPING MACHINES)**

AMCOs zinazotaka kuomba uwezeshaji huu zitatakiwa kukidhi vigezo vifuatavyo:

i. Kuwa na makusanyo ya kahawa ya parchment yasiyopungua tani 50 kwa msimu.
ii. Kueleza uwezo (Capacity) wa mashine ya kuchakata kahawa wanayoomba mfano (1Kg/saa) – 1500 Kg/hr au 2500Kg/saa).
iii. Kuwa na eneo linalofaa na kumilikiwa na AMCOs husika kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Uchakataji wa Kahawa (Coffee Processing Unit - CPU).
iv. Kuwasilisha vielelezo vinavyoonyesha uwezo wa kujenga miundombinu muhimu inayohitajika katika CPU, kama sehemu ya mchango wa AMCOS katika utekelezaji wa mpango huu na miundombinu hiyo ni pamoja na vitu vifuatavyo:-

- Meza za kuanikia kahawa;
- Ghala la kuhifadhi kahawa na ofisi;
- Kuweka miundombinu ya maji;
- Kujenga vyoo;
- Miundombinu mingine muhimu kwa uendeshaji wa CPU.

**Angalizo:** Bodi itafanya tathmini ya maombi yote yatakayowasilishwa na AMCOS zitakazokidhi vigezo zitawezeshwa kwa kununuliwa mashine mpya za kuchakata kahawa kulingana na uzalishaji na makusanyo ya Kahawa ya AMCOS husika. Maombi yote yawasilishwe kupitia kwa ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya husika kabla ya tarehe 30 Septemba, 2026.

Imetolewa na;


Primus O. Kimaryo
**MKURUGENZI MKUU,**
Bodi ya Kahawa Tanzania, (Kahawa House)
09 BR. J. K. Nyerere
S. L. P. 732, 25101 Mawenzi
**MOSHI, KILIMANJARO**
**Simu** +255 27 275 2324
**Barua Pepe:** info@coffee.go.tz;
**Wavuti:** www.coffee.go.tz


MCL Epaper Copy